

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

Simu Na: +255 (026) 2324513  
Nukushi: +255 (026) 23211027  
Barua Pepe: [ps@mawasiliano.go.tz](mailto:ps@mawasiliano.go.tz)  
Tovuti: [www.mawasiliano.go.tz](http://www.mawasiliano.go.tz)



Mji wa Serikali Mtumba,  
Mtaa wa Ujenzi,  
S.L.P. 677,  
**40470 DODOMA.**

09 Juni, 2021

**TAARIFA KWA UMMA**

Kuna taarifa ambayo inasambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu Serikali kuandaa sheria maalumu ya mtu kuwa na laini moja ya simu kwa kila kampuni ya simu ikiwa ni njia ya kulinda faragha za watu inayolenga kudhibiti uhalifu mtandaoni.

**Taarifa hizo sio za kweli.** Serikali haina mpango wa kutunga sheria mpya ya masuala ya usajili wa laini za simu. Masuala ya usajili wa laini za simu yameainishwa katika kanuni za Usajili wa laini za simu za mwaka 2020 [The Electronic and Postal Communications (SIM Card Registration) Regulations, 2020 – GN. No. 112 of 7 February, 2020] ambazo zinaeleza kuhusu idadi ya laini zinazoweza kumilikiwa pamoja na utaratibu wa kusajili laini hizo. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuzuia na kudhibiti matukio ya uhalifu mtandaoni na haikusudii kuzuia mtu kuwa na laini ya simu zaidi ya moja kama mkakati wa kudhibiti uhalifu mtandaoni.

Aidha, Serikali inakusudia kutunga sheria ya kulinda taarifa binafsi kwa lengo la kuhakikisha taarifa binafsi na faragha za watu zinalindwa.

Hivyo, Wizara inatoa rai kwa umma kutumia vyema huduma za mawasiliano na mitandao ya kijamii kwa shughuli za kiuchumi na kijamii badala ya kusambaza taarifa za uongo na kupotosha umma.

Imetolewa na;

A blue ink signature of Prisca J. Ulomi.

Prisca J. Ulomi

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari